



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

UPOTOSHAJI KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MKUU WA  
MWAKA 2020

Dar es Salaam, 11 Februari, 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imebaini kuwepo kwa taarifa ya upotoshaji kuhusu ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Taarifa hiyo potofu inasambazwa kupitia mitandao ya kijamii hasa *WhatsApp*.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Ibara ya 74(6)(b) na (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imepewa mamlaka ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kifungu cha 35B cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kikisomwa pamoja na kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292; kinaipa Tume mamlaka ya kutangaza katika gazeti la Serikali tarehe ya Uchaguzi.

Mamlaka hayo yanatekelezwa kwa mujibu wa kifungu cha 37(1)(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ambacho kinailekeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutangaza tarehe ya Uchaguzi mara baada ya kuvunjwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuwa, Bunge halijavunjwa, Tume haijatoa wala kutangaza ratiba yoyote ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Hivyo, Tume inawaomba Wananchi kuipuuza taarifa hiyo ya mtandaoni kwani si taarifa rasmi na imeandaliwa kwa nia ovu. Tume itatoa ratiba ya Uchaguzi Mkuu muda utakapowadia kulingana na matakwa ya kisheria.

Imetolewa na:

Dkt. Wilson M. Charles

Mkurugenzi wa Uchaguzi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI